



**Mradi wa uboreshaji wa Afya na Uzalishaji wa Kuku wa Kienyeji Afrika (HEPRUCA) Idara ya Tiba ya Mifugo na Afya ya Jamii Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine**

#### **TIBA ASLIA (Mmea wa Shubiri (Aloe spp))**

#### **YALIYOMO**

**Utangulizi**

**Shubiri**

**Magonjwa yatibiwayo kwa kutumia shubiri**

**Njia Sahihi ya Kutumia shubiri**

**Utafiti Unaendelea**

**Kauli Mbiu**

#### **Utangulizi**

Kuna aina nyingi sana za tiba asilia mabazo zimekuwa zikitumika na makabila mbalimbali ya Tanzania ili kupunguza ghamama kubwa za madawa ya mifugo. Mojawapo ya tiba hizi ni mimea aina ya Shubiri (aloe)

#### **Shubiri**

Jina Shubiri limetokana na neon la kiarabu lenye maana ya "Mwonjo wa kitu kichungu" Mmea huu umetokaka katika familia ya mimea ijlukanayo kwa jina la kitaalamu kama Aloeaceae ambamo uoto wake umeenea zaidi Afrika.

Majani ya mmea huu hufananishwa sana na majani ya mkonge (katani) lakini unawezwa kutofautishwa kwa maua yake ya aina mbalimbali.

Kuna takrabani aina 600 za shubiri ulimwenguni. Hupatikana katika sehemu kubwa ya Ukanda wa Afrika, Uarabuni, sehemu zenye hali ya kimediteranian na ukanda wa hari ya America. Sehemu mbalimbali za mmea huu zimekuwa zikitumiwa na wenyeweji kutibu aina mbalimbali za magonjwa.

Mradi wa Uboreshaji Afya na Uzalishaji wa Kuku wa kienyeji (HEPRUCA/TARP II 015) katika kumsaidia mkulima imefanikiwa kufanya utafiti katika mmea huu na kubainisha kuwa aina ya shubiri ijlukanayo kwa jina la kitaalamu kama Oloe secundiflora husaidia

kuponya magonjwa yatokanayo na vimelea vya bacteria kwa kiwango cha hali ya juu.

Utafiti unaendelea kuangalia aina nyinginez za mmea wa jamii hii kuweza kutibu magonjwa mbalimbali kwa kuku wa kienyeji.

Magonjwa yatibiwayo kwa kutumia shubiri Utafiti uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Umeonyesha kuwa aina hii ya shubiri (*Aloe Secundiflora*) huweza kutibu magonjwa yafuatayo kwa kuku wa kienyeji.

▪ Magonjwa yatokanayo na vimelea vya bacteria

1. Kama vile homa ya matumbo ya kuu, ugonjwa wa
2. Kuvimba macho, vidonda mbalimbali na magonjwa ya kuharisha

▪ Shubiri pia hupunguza makali ya virusi vienezavyo ugonjwa wa mdondo (Newcastle disease)

Njia sahihi ya kutumia shubiri

▪ Majani manne yaliyokomaa kwenye lita moja ya maji safi. Majani hayo yaoshwe na kukatwa vipande vidogo vidogo na kuchanganywa kwenye lita moja ya maji na kunyweshwa kuku katika kipindi kisichozidi masaa 24.

Picha: Vipande vya majani ya shubiri ndani ya maji

- Utomvu wake hutumika kutibu vidonda vitokanavyo na ndui na vidonda vya kawaida. Utomvu upakwe kwenye vidonda vilivyo wazi kwa siku tatu mfululizo asubuhi na jioni.

#### D. Utafiti Unaoendelea

Ubora wa aina nyingine za shubiri

Matibabu ya magaga (Scaly leg)

Viroboto na Chawa

Picha: Kuku mwenye magaga

Matumizi ya shubiri pamoja na chanjo katika kukinga magonjwa mbalimbali ya kuku

Matumizi bora ya shubiri kwa wakulima

Usambazaji wa vipande vya shubiri kwa wakulima.

#### Kauli Mbiu

Punguza gharama za uzalishaji, boresha afya ya kuku wa kienyeji kwa kutumia matibabu yenyе gharama nafuu. Tumia tiba asilia **SHUBIRI**